

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS
IMMIGRATION DEPARTMENT

Telegrams: "IMMIGRATION"
TELEFAX: +255 22 2850595
+255 22 2850584
TELEPHONE +255 22 2850575/6



OFISI YA KAMISHNA JENERALI,
S.L.P. 512,
Dar - es - Salaam.
Monday, 06 August 2018

**YAH: UFAFANUZI KUHUSU KUZUILIWA KWA BAADHI YA
RAIA KUONDOKA NCHINI**

Kumekuwepo na taarifa za uvumi kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii kuhusiana na watanzania kuzuiliwa kutoka nchini mpaka pale watakapofuata utaratibu wa kupata kibali cha kutoka nchini.

Taarifa hizo zimekuwa zikidai ya kwamba, kwa Mtanzania anayeishi na kufanya kazi nje ya nchi, anatakiwa apeleke mkataba wake wa kazi katika Ofisi ya Ubalazi ili ugongwe muhuri na kusainiwa, na mara anapofika nchini aende Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kupata uthibitisho (Clearance) na barua kutoka Polisi, na baadaye kutakiwa kwenda Wizara ya kazi (TAESA) na kufanya malipo ya Tsh 100,000 ili kupata kibali cha kusafiria.

Idara ya Uhamiaji, inachukua fursa hii kukanusha taarifa hizo kuwa si za kweli bali zimezushwa na mtu au kikundi cha watu kwa nia na madhumuni wanayoyajua wao.

Ukweli ni kwamba, Serikali kupitia Idara ya Uhamiaji imeimarisha udhibiti kwa kuwazuia kutoka nchini vijana na wasichana wa kitanzania wanaokwenda kufanya kazi zisizo za kiujuzi kama kazi za ndani katika baadhi ya nchi na hatimaye kujikuta wakiteswa, kunyanyaswa na kufanyishwa kazi zisizo na staha (kutumikishwa kingono) wafikapo katika nchi hizo.

Utaratibu uliopo sasa kwa kundi hili ni kwamba, kwa wale ambao tayari wapo nje ya nchi na wana mikataba ya kazi ambayo bado iko hai kwa miezi sita au zaidi, watapaswa kuonyesha nakala za mikataba hiyo na vibali vyao vya kuishi nje ya nchi pindi watakaporejea nchini kwa matembezi na kuhitaji kurudi katika nchi zao;

Ifahamike ya kwamba, zuiio hili haliwahusu raia wengine wanaokwenda nje ya nchi kwa sababu mbalimbali ilimradi wamekidhi vigezo vya kisheria na taratibu za kuondoka nchini.

Mwisho, Idara inatoa onyo kwa wale wote wanaohusika kutoa taarifa hizo za uongo endapo watabainika watachukuliwa hatua kali za kisheria. Ifahamike kwamba ni nia ya serikali kuhakikisha kwamba raia wake wanapokwenda nje ya nchi kwa shughuli mbalimbali wanakuwa salama na wanafanya kazi zao kwa uhuru bila ya manyanyaso ya aina yoyote.



ALLY M. MTANDA

**MSEMAJI WA IDARA YA UHAMIAJI,
UHAMIAJI MAKAO MAKUU,
DAR ES SALAAM**